TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MKOA WA KAGERA FUNGU 87 KWA MWAKA 2016/2017 NA MAKISIO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2017/2018

1.0 UTANGULIZI

Rasimu ya Mpango na Bajeti ya Mkoa wa Kagera kwa mwaka wa fedha **2017/2018** umezingatia mambo mbalimbali ya kisera yakiwemo;

- Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama Tawala (CCM) ya Mwaka 2015;
- Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania wakati akizindua Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba, 2015;
- Maamuzi ya Serikali ya Tano ya kuhamishia shughuli za Makao Makuu ya Serikali Dodoma;
- Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano; na
- Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mipango na Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango mwezi Novemba, 2016.

1.1 Dira ya Mkoa

Kuwa Mkoa wenye uchumi imara na endelevu unaokua kwa kiwango cha kuondoa umaskini, wenye ustawi thabiti na unaodumisha amani, utulivu na usalama.

1.2 Vipaumbele vya Mkoa wa Kagera Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018

Maeneo muhimu yatakayozingatiwa na kupewa kipaumbele katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2017/18 ni;

- UTAWAL A
- AFYA
- ELIMU
- MAPATO
- KILIMO na MIFUGO
- UVUVI na UFUGAJI NYUKI
- Maelezo kwa kina ni kama inavyoonekana katika nakala za vitabu kuanzia Uk. 3 – 6

2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA KIPINDI CHA MWAKA 2016/2017 HADI KUFIKIA MWEZI DESEMBA,2016

A. MAKISIO KIMKOA

Katika mwaka wa fedha **2016/2017** Mkoa wa Kagera (Fungu 87) umeidhinishiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutumia **Tshs. 234,791,204,000** kwa mchanganuo ufuatao:

- Shilingi **172,072,391,000** ni mishahara (PE),
- Shilingi **18,447,865,000** ni Matumizi Mengineyo (OC),
- Shilingi **16,639,554,000** Kutokana na vyanzo vyetu wenyewe (Own Sources) na
- Shilingi **27,631,394,000** za Miradi ya Maendeleo.

B: MAPOKEZI KIMKOA

Hadi mwezi Desemba, 2016, Mkoa ulikuwa umepokea jumla ya **Tshs 104,365,196,637** sawa na asilimia **44.5** ya fedha iliyoidhinishwa katika bajeti.

Kati ya fedha hizo:

- **Tshs 84,903,938,600 (49.3)** ni Mishahara (**PE**),
- **Tshs 11,313,598,037 (32.2)** ni Matumizi Mengineyo (**OC**) yakiwemo mapato ya ndani **6,863,000,367** na
- **Tshs 8,147,660,000 (29.5)** ni Miradi ya Maendeleo (**DEV**).

C: MATUMIZI KWA MKOA

- Hadi kufikia Desemba, 2016, Mkoa ulikuwa umetumia jumla ya **Tshs 100,848,452,003** sawa na asilimia **96.6** ya fedha iliyotolewa
- Kati ya fedha hizo:
    - **Tshs 84,903,938,600 (100)** ni Mishahara,
    - **Tshs 11,198,684,037 (98.9)** ni Matumizi mengineyo (OC) na
    - **Tshs 4,745,829,366 (58.3)** ni Miradi ya Maendeleo (**DEV**).

2.1 Maduhuli ya Mkoa na Makusanyo ya Halmashauri

2.1.1 MADUHULI YA MKOA:

- Katika mwaka 2016/2017 Sekretarieti ya Mkoa ilikadiria kukusanya jumla ya **Tshs 1,602,000** kama Maduhuli.
- Hadi kufikia mwezi Desemba, 2016 Sekretarieti ya Mkoa ilikuwa imekusanya jumla ya **Tshs 5,578,600** sawa na asilimia **348.2.**

2.1.2 MAKUSANYO YA HALMASHAURI

- Katika Mwaka wa Fedha **2016/2017** Halmashauri za Wilaya na Manispaa ya Bukoba zilikadiria kukusanya jumla ya **Tshs. 16,424,163,859** toka katika vyanzo vyake.
- Hadi kufikia mwezi Desemba, 2016 Halmashauri zilikuwa zimekusanya jumla ya **Tshs. 6,863,000,367** sawa na asilimia **41.8** ya makusanyo
- **Tshs 2,170,195,869** zilipelekwa katika miradi sawa na **39.5%** ya mapato halisi yaliyokusanywa.

- Aidha **Tshs 327,586,693** sawa na asilimia **6.0** zimetolewa kwa Vikundi **133** vya wanawake na vijana kama ifuatavyo;

- Muleba **(21)**, Kyerwa **(10)**, Missenyi **(38)**, Karagwe **(52)**, Bukoba DC **(3)**, Biharamulo **(8**), Bukoba MC **(13)** na Ngara **(14)**
- **Jedwali Na. 1 uk. 8 linaonesha mchanganuo wake.**

2.1.3 Sababu za Kutokufikia Malengo na Hatua Zilizochukuliwa

a) **Sababu na Kutokufikia Malengo**

➢ Zimeainishwa vizuri katika nakala ya kitabu chetu ukurasa wa 8 – 9

b) **Hatua Zilizochukuliwa**

➢ Zimeainishwa vizuri katika nakala ya kitabu chetu ukurasa wa 9

2.2 MAPATO YATOKANAYO NA RUZUKU

2.2.1Fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Sekretarieti ya Mkoa (Matumizi ya Kawaida)

Mgawanyo wa **Tshs. 8,540,603,000** za Matumizi ya Kawaida katika Sekretarieti ya Mkoa ni:

- **Tshs. 6,956,306,000** kwa Mishahara na
- **Tshs.1, 584,297,000** matumizi mengineyo (OC).
- Hadi kufikia mwezi Desemba, 2016 jumla ya **Tshs 4,504,536,270** zilikuwa zimetolewa sawa na **52.7%** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati yake;
- **Tshs. 3,259,012,600**(**46.8%)** ni Mishahara (PE),
- **Tshs. 1,245,523,670(78.6%)** ni Matumizi Mengineyo (OC).
- Kufikia kipindi hicho jumla ya **Tshs 4,403,973,270** zilikuwa zimetumika sawa na **97.8%** ya fedha iliyotolewa. Kati yake;
- **Tshs 3,259,012,600** (**100%)** ni Mishahara (PE),
- **Tshs 1,144,960,670 (91.9%)** ni Matumizi Mengineyo (OC).

2.2.2 Fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Halmashauri (Matumizi ya Kawaida)

➢ Halmashauri za Mkoa wa Kagera zimeidhinishiwa kutumia jumla ya **Tshs 181,979,653,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo;

➢ **Tshs 165,116,085,000** ni kwa ajili ya Mishahara (**PE**) na

➢ **Tshs 16,863,568,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (**OC**).

➢ Hadi kufikia mwezi Desemba, 2016 jumla ya **Tshs 84,850,000,000** zilikuwa zimetolewa sawa **47%** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati yake

➢ **Tshs. 81,644,926,000** (**49.4%)** ni Mishahara (PE),

- **Tshs. 3,205,074,000(19%)** ni Matumizi ya Mengineyo (OC).
- Kufikia kipindi hicho jumla ya **Tshs 84,835,649,000** sawa na asilimia **100** ya fedha iliyotolewa zilikuwa zimetumika. Kati yake;
- **Tshs 81,644,926,000** (**100%)** ni Mishahara (PE),
- **Tshs 3,190,723,000** (**99.6%)** ni (OC).

2.2.3 Orodha ya shughuli muhimu zilizotekelezwa kwa kifupi – Matumizi ya Kawaida 2016/2017 hadi Desemba, 2016

a) **Sekretarieti ya Mkoa**

Maelezo kwa kina yanapatikana katika ukurasa wa 12 katika kitabu chetu

b) **Halmashauri za Wilaya na Manispaa ya Bukoba**

Maelezo kwa kina yanapatikana katika ukurasa wa 13 katika kitabu chetu

2.3 Fedha za Maendeleo

2.3.1 Fedha zilizoidhinishwa kwa Sekretarieti ya Mkoa

- Mwaka wa fedha **2016/2017** Sekretarieti ya Mkoa imeidhinishiwa **Tshs. 1,446,425,000** ambapo;
- **Tshs.1,266,995,000** ni fedha za ndani (Local Funds)
- **Tshs. 179,430,000** ni fedha za nje (Foreign Funds).
- Hadi kufikia mwezi Desemba, 2016 Sekretarieti ya Mkoa ilipokeaTshs 627,402,000 sawa na 43.4% ya fedha zilizoidhinishwa
- Hadi kufikia kipindi hicho, Sekretarieti ya Mkoa ilitumia Tshs 31,163,366 sawa na 5% ya fedha zilizopokelewa.
- Jedwali 3. Uk. 14 - 16 linaonesha Miradi ya Sekretarieti ya Mkoa iliyoidhinishwa pamoja na Mapokezi ya Fedha 2016/2017

2.3.2. Fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Halmashauri,

- Zimeidhinishiwa **Tshs 36,266,816,000** ambapo;
    - **Tshs 15,743,580,000** ni fedha za nje na
    - **Tshs 20,523,236,000** ni fedha za ndani.
- Hadi kufikia mwezi Desemba, 2016, mapokezi ni **Tshs 7,520,258,000** sawa na **20.7%**.

Hadi kufikia kipindi hicho, matumizi ni **Tshs 4,714,666,000** sawa na **62.7%** ya mapokezi

- **Jedwali Na. 4 uk. 17 linaonesha Fedha za Miradi – Halmashauri 2016/2017**

2.3.3 Orodha ya shughuli muhimu zilizotekelezwa kwa kifupi – Miradi ya Maendeleo 2016/2017 hadi mwezi Desemba, 2016

- Maelezo kwa kina kuhusu Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri za Wilaya na Manispaa ya Bukoba yanapatikana uk.18 katika kitabu chetu

2.4 Changamoto na Mikakati ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2016/2017 angalia Uk. 19 – 20 katika nakala ya kitabu

3.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA 2017/2018

3.1 Maduhuli ya Mkoa na Makusanyo ya Halmashauri

- Mkoa unaomba kuidhinishiwa makusanyo ya **Tshs. 18,823,989,492** sawa na ongezeko **13.1%** ukilinganisha na mwaka huu (2016/17) ambapo;
- **Tshs. 12,607,000** ni maduhuli ya Sekretarieti ya Mkoa
- **Tshs. 18,811,382,492** ni makusanyo ya mapato ya ndani.
- Kiasi cha **Tshs. 9,637,969,556** kimetengwa toka katika mapato ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo
- Kiasi cha T**shs 1,380,778,946** kimetengwa kwa ajili ya mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana
- **Jedwali Na. 5 uk. 21 linaonesha Makadirio ya Makusanyo ya Vyanzo vya Ndani vya Halmashauri kwa mwaka 2017/2018**

3.2 Mapato Yatokanayo na Ruzuku

3.2.1 Matumizi ya Kawaida (Sekretarieti ya Mkoa)

- Sekretarieti ya Mkoa inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shs. 10,419,596,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo;
- **TShs. 8,733,338,000** ni Mishahara (PE) na
- **TShs. 1,686,258,000** ni Matumizi Mengineyo (OC).
- **Jedwali Na. 6 uk.22 linaonesha Makisio ya Mishahara na Matumizi Mengineyo – Sekretarieti ya Mkoa 2017/2018**

3.2.2 Matumizi ya Kawaida (Halmashauri)

- Halmashauri za Wilaya na Manispaa ya Bukoba zinaomba kuidhinishiwa T**Shs. 251,261,574,189** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo;
  - T**Shs. 232,452,695,189** ni Mishahara (PE) na
  - T**Shs. 18,808,879,000** ni Matumizi ya Mengineyo (OC).
  - **Jedwali Na. 7 uk. 23 linaonesha Makisio ya Matumizi ya Kawaida – Halmashauri 2017/2018**

3.3 Fedha za Maendeleo

3.3.1 Sekretarieti ya Mkoa

- Sekretarieti ya Mkoa inaomba kuidhinishiwa T**Shs. 2,910,170,000** ambapo T**Shs. 389,530,000** ni fedha za nje na **Shs. 2,520,640,000** ni fedha za ndani.
- **Jedwali Na. 8 uk. 23 – 24 ni mchanganuo wake**

3.3.2 Halmashauri za Wilaya na Manispaa

- Halmashauri zinaomba kuidhinishiwa T**Shs. 51,885,902,303** ambapo T**Shs. 21,950,170,591** ni fedha za nje na **Shs. 29,935,731,712** ni fedha za ndani.
- **Jedwali Na. 9 uk. 24 ni mchanganuo wa Makisio ya fedha**

4.0 MAOMBI MAALUM

1. Mkoa unawasilisha ombi maalum la kutizamwa kipekee katika mgao wa "**ceilings**" hasa za maendeleo ili kuweza kurejesha hali ya uharibifu mkubwa wa miundombinu uliotokea katika Mkoa wetu kutokana na tetemeko lililotokea mnamo tarehe **10 Septemba, 2016** majira ya **saa 9** za alasiri.

   - Maelezo kwa kirefu ni kama yanavyoonekana katika ukurasa wa 25 katika nakala za vitabu

2. Ununuzi wa gari la Mhe. Mkuu wa Mkoa – 350,000,000
3. Magari 7 ya makatibu Tawala wa Wilaya – 560,000,000
4. Vyombo vya usafiri (pikipiki 27) kwa ajili ya maafisa Tarafa – 189,000,000

- **Jumla maombi maalum – 1,099,000,000**

5.0 HITIMISHO

- Mpango na Bajeti ya Mkoa wa Kagera umewasilishwa na kujadiliwa katika vikao mbalimbali vya kisheria kabla ya kuwasilishwa katika Kikao hiki.

- Vikao hivyo vimefanyika katika ngazi ya Mamlaka za Serikali vilivyojumuisha Kamati zote za Kudumu za Halmashauri, Mabaraza ya Wafanyakazi yote, Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC) na Mabaraza ya Madiwani.

- Aidha katika ngazi ya Mkoa Baraza la Wafanyakazi limeketi tarehe **01/03/2017** na leo ni Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), hivyo taratibu zote za kisheria zimezingatiwa.